# Prisoners Sentenced to Death in Tanzania:

# A New Decision by the African Court Affects Your Case




I've seen you've been working on something, what are you writing?
I am filling out a petition to the African Court because of their recent decision in the case of Rajabu.
Oh, what's that about?
In Tanzania, if you're convicted of murder, you're automatically sentenced to death.
Yes, that's what happened to me.
A Tanzanian prisoner named Rajabu thought that this was wrong, so he brought a case to the African Court on Human and Peoples' Rights.
Mr. Rajabu, the court convicts you of murder.
Under Tanzanian law, anyone convicted of murder must be given the death penalty.
Your background isn't relevant.
The court hereby sentences you to death.
Death? Don't I get to tell you about my background?
... RAJABU THOUGHT THIS WAS WRONG, SO HE FILED AN APPLICATION WITH THE AFRICAN COURT ON HUMAN AND PEOPLES' RIGHTS....










**TANZANIA HAS SAID THAT INDIVIDUALS MAY NO LONGER SUBMIT PETITIONS TO THE AFRICAN COURT.**

**THIS DECISION TAKES EFFECT ON NOVEMBER 20TH, 2020.**

# YOU MUST SUBMIT YOUR APPLICATION BY

# NOVEMBER 20TH, 2020


That doesn't seem like much time. I don't even know how to start.
If you need help, there is an organization that is willing to help inmates on death row file petitions to the African Court. Volunteer lawyers will provide applications to the prison that you can fill out and send to the African Court.
THE PAN AFRICAN LAWYERS UNION
PALU
Pan African Lawyers Union
We are PALU lawyers.
We are volunteer lawyers, so our services are FREE. We are asking the African Court to clarify that *Rajabu* applies to everyone. But you can also file your own application.
Well, is it guaranteed that I will get off death row?
It's not guaranteed. But isn't it better to try and have the possibility of life beyond prison?
You're right, I will try and file an application!

# Wafungwa Waliohukumiwa Kifo Nchini Tanzania:

# Uamuzi Mpya wa Mahakama ya Afrika Unaathiri Kesi Yako




Naona umekuwa ukifanya jambo fulani, unaandika nini?
Najaza ombi litakalotumwa kwa Mahakama ya Afrika kwa sababu ya uamuzi wao wa hivi karibuni katika kesi ya Rajabu.
Ah, ni kuhusu nini?
Nchini Tanzania, ukipatwa na hatia ya mauaji, basi moja kwa moja unahukumiwa kifo.
Ndiyo, hivyo ndivyo ilitokea kwangu.
Mfungwa mmoja nchini Tanzania anayeitwa Rajabu aliona kwamba hilo si sawa, hivyo alipeleka kesi katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu.
Bw. Rajabu, Mahakama imekupata na hatia ya mauaji.
Chini ya sheria ya Tanzania, mtu yeyote mwenye hatia ya mauaji lazima ahukumiwe adhabu ya kifo. Usuli wako hauzingatiwi.
Kwa hiyo Mahakama inakuhukumu kifo.
Kifo? Sipati fursa ya kueleza kuhusu usuli wangu?
. . . RAJABU ALIONA KWAMBA HILO SI SAWA, HIVYO AKAFUNGUA OMBI KATIKA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU . . .










**TANZANIA IMESEMA KUWA MTU MMOJAMMOJA HAWEZI TENA KUWASILISHA MAOMBI KATIKA MAHAKAMA YA AFRIKA.**

**UAMUZI HUU UNAANZA KUTEKELEZWA NOVEMBA 20, 2020.**

# UNAPASWA KUWASILISHA OMBI LAKO KABLA YA

# NOVEMBA 20, 2020


Huo hauonekani kuwa muda mrefu. Hata sijui mahali pa kuanzia.
Ikiwa unahitaji msaada, kuna shirika ambalo liko tayari kuwasaidia wafungwa ambao wamehukumiwa kifo kufungua maombi katika Mahakama ya Afrika. Wanasheria wa kujitolea watakuletea maombi hayo gerezani ambapo unaweza kujaza na kutuma kwa Mahakama ya Afrika.
UMOJA WA WANASHERIA WA PAN AFRICAN
PALU
Pan African Lawyers Union
Sisi ni wanasheria wa PALU.
Sisi ni wanasheria wa kujitolea, hivyo tunatoa huduma BURE. Tunaiomba Mahakama ya Afrika ifafanue kwamba *Rajabu* anawakilisha kila mtu. Lakini unaweza pia kufungua ombi lako mwenyewe.
Sasa, kuna uhakika kwamba nitaondolewa kwenye orodha ya waliohukumiwa kifo?
Hakuna uhakikisho. Lakini si bora kujaribu na kupata uwezekano wa kuwa na kifungo cha maisha gerezani?
Uko sahihi, nitajaribu na kujaza ombi!